

## **SURA YA KWANZA**

### **1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi imeandaa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2018/2019 kwa kuzingatia Maelekezo na Mwongozo wa Kitaifa, Mipango Shirikishi ya Jamii, Mpango Mkakati wa Halmashauri wa Mwaka 2017/2018 - 2021/2022 na Vipaumbele vya Halmashauri. Aidha tutaendelea kutekeleza shughuli muhimu ambazo zinalenga katika kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) ili kuleta Maendeleoya Kiuchumi na ya Kijamii kama inavyosisitizwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka 5 awamu ya Pili 2016/17- 2020/21, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ya 2030, pia imezingatia "Tanzania Development Vision 2025". Aidha Mgawanyo wa fedha utaendelea kuzingatia maeneo ya vipaumbele ambavyo vitaleta msukumo katika Uchumi na Huduma Bora za Jamii na Utawala bora. Bajeti hii imeandaliwa kwa Mujibu wa Kifungu Na 21 cha Sheria ya bajeti Na 11 ya Mwaka 2015 pamoja na Kanuni zake.

### **1.1 MAENEO YALIYOZINGATIWA KATIKA MGAWANYO WA RASILIMALI KITAIFA**

#### **(a) Matumizi ya Mishahara**

Katika kutenga fedha za Mishahara imezingatia watumishi waliopo, ajira mpya, upandishaji wa vyeo, nyongeza za mishahara na michango ya kisheria. Katika kuandaa bajeti ya mishahara yafuatayo yatazingatiwa:-

- Kutumia mfuo wa usimamizi wa taarifa za rasilimali watu kuandaa mipango na bajeti ya mwaka 2018/2019
- Malipo ya mishahara yazingatie maelekezo ya waraka wa Hazina Na.2 w Mwaka 2017 unaoelekeza utumiaji wa Government Salary Payments Platforms (GSPP)
- Posho za kukaimu nafasi za uongozi zinazosubiri uteuzi zilipwe kupitia bajeti za mishahara. Aidha posho za kukaimu nafasi za uongozi zinazotokana na ugonjwa, likizo na safari zitaendelea kukasimiwa katika bajeti ya matumizi mengineyo
- Kuendelea kufanya uhakiki wa takwimu za watumishi na kuondoa wasiostahili pamoja na kufanya tathmini ya mahitaji ya watumishi kwa mujibu wa ikama

- Kutenga bajeti kwa ajili ya michango ya kisheria pamoja na kiinua mgongo kwa watumishi wenye ajira za mikataba

### **(b) Matumizi mengineyo (OC)**

Halmashauri imetenga fedha kwa ajili ya matumizi yasiyoepukika pamoja na majukumu ya msingi ikiwemo kulipa madeni mbalimbali ya watumishi pamoja na madeni ya wazabuni na watoa huduma mbalimbali ili kuepuka kulimbikiza madeni na gharama za kulipa riba.

### **(c) Fedha za Maendeleo**

Katika ugawaji wa rasilimali katika Miradi ya Maendeleo maeneo yatakayopata fedha ni yafuatayo:-

- Miradi ambayo haijakamilika inaendelea kutekelezwa ambayo itapunguza au kuondoa kero za Wananchi.
- Kufanya uthamini wa ardhi na mali pamoja na kulipa fidia katika maeneo ya uwekezaji, ujezi wa hospitali ya wilaya
- Kufanya tafiti ya vyanzo vya makusanyo ya ndani ili tuweze kupata uhalisia wa kila chanzo
- Kuwezesha uwanzishaji wa viwanda vidogovidogo na upatikanaji wa teknolojia rahisi na nafuu kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii na Ushirika
- Miradi yenye Wakandarasi na ambayo Mikataba yake imewekewa saini na wafanyabiashara waliotoa huduma kwa Serikali na Halmashauri.
- Kukamilisha miradi ambayo imeanzishwa na jamii na ambayo inaondoa kero za Wananchi
- Kuandaa miradi ya maendeleo hususani idara ya maji kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Halmashauri wa Mwaka 2017/2018 – 2021/2021
- Kutenga fedha kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji na tathmini

#### **(d) Fedha za Mapato ya Ndani**

- (i) Pia serikali imesisitiza kuwa fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri matumizi yake yatagawanyika kama ifuatavyo:-
- 40% zitaelekezwa katika Miradi ya Maendeleo
  - 60% kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida pamoja na ulipaji wa posho za Waheshimiwa Madiwani pamoja na uendeshaji wa Vikao vya Kisheria katika Halmashauri. Mapato ya Halmashauri yatakatiwa risiti ya mfumo wa kielektroniki.
  - 10% kwa ajili ya; mfuko wa maendeleo wa vijana (4%), wanawake (4%) na watu wenye ulemavu (2%)

#### **(e) Masuala Mtambuka**

Katika Maandalizi ya Mipango na Bajeti ya Mwaka 2018/19 , Halmashauri imezingatia Masuala Mtambuka kwa kila sekta yahasuyo:-

- Lishe na kinga, HIV/AIDS na Virusi vya Ukimwi, Mazingira, Ulemavu, Wazee, Ulinzi wa Mtoto, Vijana

#### **(f) Kuongeza Ajira na Kuinua Uchumi**

Katika kuwezesha jamii Kiuchumi, Halmashauri kupitia Mapato yake ya ndani imetenga asilimia 8% kwa ajili ya kuviwezesha vikundi vya wanawake na vijana vyenye kuleta tija ili kuweza Kukuza Uchumi katika Ngazi ya jamii na asilimia 2% kwa ajili ya walemavu. Vilevile Halmashauri imelenga kukuza Uchumi kwa Wananchi kupitia Maeneo yaliyotengwa ya "Special Economic Zone" (SEZ) yaliyopo katika Kata ya Bulemeji na Ukiriguru ambapo vitaanzishwa Viwanda Vidogo, Kati na Vikubwa.

#### **(g) Uendeshaji wa vikao vya kisheria**

Halmashauri inahakikisha kuwa Vikao vya Kisheria vinafanyika kuanzia Ngazi ya Kijiji, Kata na hatimaye Halmashauri kwa Mujibu wa Miongozo, Taratibu, Kanuni na Sheria.

## 1.2 HATUA ZA KUDHIBITI MATUMIZI NA KUPUNGUZA GHARAMA

Katika Mpango wa Mwaka 2018/2019 Halmashauri imepanga kudhibiti Matumizi na kupunguza gharama kama ifuatavyo:-

- i. Kupunguza gharama za Matumizi yasiyokuwa ya lazima ikiwemo Sherehe za Kitaifa, Posho za vikao, Uchapishaji wa Fulana, Kofia, Mikoba, Safari za Nje, Mafunzo ya muda mfupi Nje ya Nchi na Ununuzi wa Samani Nje ya Nchi.
- ii. Kuhakikisha Mikutano yote ikiwa ni pamoja na Mikutano ya Bodi, Mafunzo, Warsha na semina inafanyika katika Kumbi za Serikali na Taasisi za Umma.
- iii. Kuhakikisha thamani halisi ya fedha inazingatiwa katika manunuzi ya bidhaa, huduma na ujenzi

## 1.3 MALENGO YA WILAYA NA VIPAUMBELE KWA MWAKA 2018/2019

Kulingana na Mwongozo wa Mpango na Bajeti 2018/2019, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi imeweka vipaumbele vyake ambavyo vinalenga kujibu matarajio ya Serikali ya Awamu ya Tano Kulingana na Mwongozo ulitolewa, Vipaumbele vya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ni vifuatavyo:

| NA | Vipaumbele   |
|----|--|
|    | <b>Afya</b>  |
| 1. | Kuwezesha ukarabati wa chumba cha upasuaji katika hospitali ya wilaya ya Misungwi, Mbarika na Mwawile                                |
| 2. | Kuwezesha Ujenzi wa jengo la Huduma za bima ya Afya katika Hosptali ya Wilaya ya Misungwi  |
| 3. | Kuwezesha ukamilishaji wa ujenzi wa kituo cha Afya kata ya Mondo   |
| 4. | Kuwezesha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa ajili ya dharula na majanga katika vituo 46 vya kutolea huduma ya afya |
| 5. | Upanuzi wa kituo cha Afya Koromije   |
| 6. | Kumalizia ujenzi wa OPD katika zahanati ya Ng'obo, Lutalutale, Mapilinga ,Nyamatala  |
| 7. | Ujenzi wa nyumba ya mganga (two in one) katika zahanati ya Nyangh'omango, Mwagimagi, Ibongongoya B                                   |
|    | <b>UTAWALA</b>   |
| 8. | Ujenzi wa Jengo la Halmashauri ya Wilaya   |

|     |  |
|-----|--|
| 9.  | Ujenzi wa ofisi 5 za kata  |
| 10. | Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kielektroniki (LGRCIS) kwa kununua mashine za kukusanyia mapato POS kutoka POS 70 hadi POS 115, hivyo kuondoa upungufu uliopo, hali hii itawezesha mashine kupatikana kwa kila kijiji katika vijiji 113, Kuongeza mtandao wa mfumo (LAN) pia kuendelea kutoa mafunzo kwa watumiaji. |
| 11. | Kuendelea kufanya upembuzi yakinifu wa vyanzo vyote vya mapato ya ndani ili kuiwezesha Halmashauri kuvisimamia vyanzo hivyo kikamilifu na pia kuwezesha uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato.  |
| 12. | Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji uhifadhi na uboreshaji wa takwimu katika sekta zote.  |
|     | <b>Ardhi</b>   |
| 13. | Kupima na kutoa Hati Miliki za Wamiliki wa Viwanja katika Miji ya Misungwi, Usagara na Misasi.   |
| 14. | Kutatua Migogoro Ardhi katika Tarafa za Misungwi, Usagara, Inonelwa na Mbarika.  |
|     | <b>Elimu msingi</b>  |
| 15. | Kuwezesha ukamilishaji na ukarabati wa vyumba vya madarasa katika shule 10 za msingi   |
| 16. | Kuwezesha ukamilishaji/ukarabati wa vyoo katika shule za Msingi 139  |
| 17. | Kuhamasisha Jamii katika kata 27 ili kuweza kuongeza Vyumba vya Madarasa kulingana na upungufu uliopo.   |
|     | <b>Elimu sekondari</b>   |
| 18. | Kukarabati vyumba 20 vya madarasa katika shule za sekondari Misasi na Sanjo  |
| 19. | Ukamilishaji wa maabara 9 katika shule za sekondari za Mbarika, Paulo Bomani na Kasololo   |
| 20. | Kuhamasisha Jamii katika kata 27 ili kuweza kuongeza Vyumba vya Mdarasa kulingana na upungufu uliopo   |
| 21. | Kuanzisha mpango wa chakula katika shule 23 za Sekondari   |
| 22. | Ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu ya kidato cha tano katika shule za sekondari Misasi na Paulo Bomani  |
| 23. | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Miundombinu katika Shule Mpya ya Sekondari Gulumungu   |
|     | <b>Mazingira</b>   |
| 24. | Kuimarisha kitalu cha miti cha Wilaya kwa kuotesha na kupanda miti 1,500,000 ya aina mbalimbali katika maeneo ya taasisi   |
| 25. | Kuimarisha usafi wa mazingira katika miji ya Misasi, Misungwi, Usagara na Mabuki kwa kusambaza vifaa vya kutupia taka na kutoa elimu juu ya usafi wa mazingira   |
|     | <b>M/Jamii</b>   |
| 26. | Kuvipatia mkopo vikundi 20 vya wanawake vya uzalishaji wa kiuchumi   |

|     |   |
|-----|---|
| 27. | Kuvipatia mkopo vikundi 35 vya vijana wazalishaji wa jamii  |
|     | <b>Kilimo</b>   |
| 28. | Kuhamasisha jamii kuongeza uzalishaji wa mazao ya Chakula na Biashara angalau kila kaya kulima eka 1 ya pamba na ekari 1 ya Mtama, Mpunga na Alizeti                          |
| 29. | Kuwezesha uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula kwa kununua trekta 2 na pikipiki 27  |
| 30. | Kuhamasisha kilimo cha Umwagiliagi kwenye zao la Mpunga kwa maeneo yaliyopo kandokando ya Ziwa ambayo ni Nange, Mwalogwabagole,   |
| 31. | Kuboresha miundombinu ya Umwagiliagi katika miradi ya umwagiliaji ya Igenge, Nyashidala, Igongwa, Ilujamate, Nyambeho, Mbarika ili wakulima waweze kulima kilimo chenye Tija. |
| 32. | Kuwezesha ushiriki wa maonyesho ya Nanenane   |
|     | <b>Mifugo</b>   |
| 33. | Kukarabati joshu la Mwamimagi   |
| 34. | Kuwezesha chanjo za Mifugo kwa ajili ya kuzuia magonjwa ya Mifugo na yatokayo kwa Mifugo kwenda kwa Binadamu.   |
| 35. | Kuendelea na zoezi la ufuatiaji na Utambuzi wa Mifugo ili kuthibiti Mifugo inayohamia kiholela  |
| 36. | Uwezeshwaji wa huduma ya uhamilishaji katika vijiji vya Bukumbi na Misungwi   |
| 37. | Kuimarisha huduma za Ugani katika kata zote 27  |
| 38. | Kuzuia uvuvi haramu kwa kuendesha doria za mara kwa mara na kuendeleza ufugaji wa samaki  |

## SURA YA PILI

### 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI 2017/2018

#### 2.1 Fedha zilizoidhinishwa 2017/2018

Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi iliidhinishwa Kutumia kiasi cha Tshs. 41,131,928,000 ikiwemo Tshs. 1,359,562,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, Tshs. 2,062,378,000 Mapato ya Ndani, Tshs. 29,926,083,000 Mishahara na Tshs. 7,783,905,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

#### Jedwali Na. 1 Muhtasari wa Fedha zilizoidhinishwa kwa Mwaka 2017/2018

| Eneo                             | Bajeti iliyoidhinishwa 2016/2017 |
|----------------------------------|----------------------------------|
| Mapato ya vyanzo vya ndani       | 2,062,378,000                    |
| Mishahara                        | 29,926,083,000                   |
| Matumizi ya Kawaida (OC)         | 1,359,562,000                    |
| <b>Jumla matumizi ya kawaida</b> | <b>33,348,023,000</b>            |
| <b>Miradi ya maendeleo</b>       |                                  |
| Fedha za Ndani                   | 3,088,138,000                    |
| Fedha za Nje                     | 4,695,767,000                    |
| <b>Jumla ndogo Maendeleo</b>     | <b>7,783,905,000</b>             |
| <b>JUMLA KUU</b>                 | <b>41,131,928,000</b>            |

#### 2.2 Fedha zilizopokelewa hadi robo ya Pili (Julai 2017 - Novemba 2017)

Hadi kufikia 30 Novemba, 2017 Halmashauri imepokea Tshs. 14,447,501,149 sawa na asilimia 35.19 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya hizo shs. 11,221,892,500 ni Mishahara, shs. 277,806,851 Matumizi Mengineyo na shs. 2,947,801,798 ni fedha za Maendeleo.

#### Jedwali Na. 2: Mapato na Matumizi kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Novemba 2017

| Eneo                                   | Bajeti idhinishwa     | Fedha zilizopokelewa hadi Novemba, 2017 | %            | Matumizi hadi Novemba 2017 | %            |
|--|-----------------------|---|--------------|----------------------------|--------------|
| <b>Matumizi ya kawaida</b>             |                       |   |              |                            |              |
| Mishahara                              | 29,926,083,000        | 10,767,158,032                          | 35.98        | 10,757,126,900             | 99.91        |
| Matumizi mengineyo                     | 1,359,562,000         | 169,010,000                             | 12.43        | 115,840,312                | 68.54        |
| <b>Jumla ndogo matumizi ya kawaida</b> | <b>31,285,645,000</b> | <b>10,936,168,032</b>                   | <b>34.96</b> | <b>10,872,967,212</b>      | <b>99.42</b> |
| <b>Fedha za maendeleo</b>              |                       |   |              |                            |              |
| Fedha za nje                           | 5,783,879,500         | 1,831,046,882.05                        | 20.40        | 1,725,056,491              | 94.21        |
| Fedha za ndani                         | 3,437,452,500         | 1,180,153,317.53                        | 53.27        | 974,241,258                | 82.55        |
| <b>Jumla ndogo maendeleo</b>           | <b>9,021,332,000</b>  | <b>3,011,200,199.58</b>                 | <b>33.38</b> | <b>2,699,297,749</b>       | <b>89.64</b> |
| <b>JUMLA KUU</b>                       | <b>40,306,977,000</b> | <b>13,947,368,231.58</b>                | <b>34.60</b> | <b>13,572,264,961</b>      | <b>97.31</b> |

### 2.3 Matumizi 2017/2018:

Hadi Novemba 2017, shs. **10,767,158,032** zilitumika kwa ajili ya Misahahara, Matumizi Mengineyo na Miradi ya Maendeleo. Mishahara ikiwa ni shs. **10,767,158,032** sawa na 99.91% ya fedha za Mishahara zilizopokelewa, Matumizi Mengineyo shs. 115,840,312 sawa na 68.54% ya fedha zilizotolewa na miradi ya maendeleo shs. **2,699,297,749** sawa na 89.64 ya fedha zilizotolewa.

### 2.4 Makusanyo ya Mapato ya Ndani 2017/2018

Katika Mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ya Wilaya ilikadiria Kukusanya Maduhuli ya Shs. 2,062,378,000 kutoka vyanzo vya ndani. Mapato haya yanatokana na ada, ushuru mbalimbali, faini, leseni nk. Hadi kufikia Novemba 2017, Tshs. **653,160,439.45** zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia **31.67** ya Makadirio ya Mwaka Mzima.

**Jedwali Na. 3: MAPITIO YA UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI KUENZIA 2016/2017 HADI 2017/2018**

| KIFUNGU | MAELEZO YA KASMA                    | MAKUSANYO HALISI 2016/2017 | MAKISIO 2017/2018 | Makusanyo 2017/18 (Novemba 2017) | %      |
|---------|-------------------------------------|----------------------------|-------------------|----------------------------------|--------|
| 140283  | Ada ya Zabuni                       | 7,650,000                  | 13,000,000        | 1,900,000                        | 14.62  |
| 140291  | Ushuru wa Magulio                   | 36,259,287                 | 48,600,000        | 14,005,200                       | 28.82  |
| 140390  | Ushuru wa Mnada wa mifugo           | 159,265,403                | 145,920,000       | 72,603,200                       | 49.76  |
| 140349  | Ushuru wa Machinjio                 | 12,894,013                 | 21,570,000        | 6,225,850                        | 28.86  |
| 140351  | Ada ya Matangazo                    | 23,251,653.47              | 37,151,000        | 10,520,000                       | 28.32  |
| 140392  | Ushuru wa Stendi Misungwi/Nyashishi | 84,175,468                 | 162,360,000       | 58,461,000                       | 36.01  |
| 140398  | Ushuru wa Mialo                     | 5,329,007                  | 6,480,000         | 1,016,000                        | 15.68  |
| 110806  | Ushuru wa Pamba                     | 39,043,900                 | 56,250,000        | 16,000,000                       | 28.44  |
| 140383  | Faini mbalimbali/Mapato mengineyo   | 6,608,900                  | 15,000,000        | 86,623,935.10                    | 577.49 |
| 110814  | Ushuru wa mazao                     | 162,059,757                | 80,520,000        | 40,778,800                       | 50.64  |
| 110851  | Ushuru wa huduma                    | 13,725,482.91              | 153,200,000       | 27,584,057.85                    | 18.01  |
| 140292  | Ushuru wa soko jipya/kuu            | 46,691,116.17              | 21,060,000        | 5,363,000                        | 25.47  |
| 140408  | Ushuru wa Vibanda/Nyumba            | 16,487,500                 | 95,880,000        | 10,400,000                       | 10.85  |
| 140369  | Leseni za uvuvi                     | 19,820,000                 | 20,328,000        | 966,500                          | 4.75   |
| 140370  | Ushuru wa vinywaji vikali           | 20,709,006                 | 4,252,000         | 1,779,000                        | 41.84  |
| 140375  | Ushuru wa Kokoto na Mchanga         | 3,276,000                  | 140,400,000       | 39,510,100                       | 28.14  |
| 140395  | Bili za maji mjini                  | 32,920,400                 | 190,320,000       | 86,079,844.50                    | 45.23  |
| 140380  | Vibali vya ujenzi                   | 1,915,000                  | 10,440,000        | 1,270,000                        | 12.16  |
| 140381  | Leseni za vyombo vya uvuvi          | 7,516,494                  | 6,426,000         | 634,000                          | 9.87   |



|        |                                   |                         |                      |                       |              |
|--------|-----------------------------------|-------------------------|----------------------|-----------------------|--------------|
| 140289 | Upimaji wa viwanja                | 57,522,563              | 200,000,000          | 12,964,300            | 6.48         |
| 140371 | Leseni za biashara                | 45,182,140              | 63,000,000           | 24,521,700            | 38.92        |
| 140353 | Shughuli za madini                | 18,109,000              | 137,520,000          | 19,007,000            | 13.82        |
| 110801 | Kodi ya majengo                   | 22,569,025              | 136,400,000          | 31,480,000            | 23.08        |
| 140505 | Mfuko wa afya(cost sharing/CHF)   | 190,603,020.56          | 208,000,000          | 73,761,252            | 35.46        |
|        | Ada za leseni za pikipiki         | 33,000                  | 4,601,000            | 1,730,000             | 37.60        |
|        | Ada za michezo na utamaduni       | 140,000                 | 10,500,000           | 60,000                | 0.57         |
|        | Ushuru wa maegesho                | -                       | 37,800,000           | -                     | -            |
|        | Ushuru wa nyumba za kulala wageni | 6,396,500               | 9,000,000            | 2,006,400             | 22.29        |
|        | Ushuru wa minara ya simu          | 6,600,000               | 26,400,000           | 5,909,300             | 22.38        |
|        | Mapato Mengineyo                  | 14,411,600              | -                    | -                     | -            |
|        | <b>Jumla Mapato ya ndani</b>      | <b>1,330,197,946.11</b> | <b>2,062,378,000</b> | <b>653,160,439.45</b> | <b>31.67</b> |

### **Changamoto katika ukusanyaji wa mapato ya ndani 2017/2018**

- Baadhi ya vyanzo ukusanyaji wake ni wa msimu mfano ushuru wa pamba, ushuru wa mialo na ushuru wa mazao
- Upungufu wa mashine za kukusanyia mapato (POS) zinahitajika 113 zilizopo ni 37
- Uelewa mdogo wa walipa kodi au ushuru

## 2.5 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO 2017/2018

Katika Mwaka wa Fedha 2017/2017, Halmashauri iliidhinishiwa shs. 9,021,332,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Maendeleo. Kati ya hizo shs. 3,437,452,500 ni fedha za ndani na shs. 5,783,879,500 ni fedha za nje.

Hadi mwezi Desemba 2017, Jumla ya Tshs. 3,011,200,199.58 zilikuwa zimetolewa na kiasi cha Tshs. 2,699,297,748.53 kilikuwa kimetumika kama inavyooneshwa hapa chini:-

### Muhtasari wa Mapokezi na Matumizi ya Fedha za Maendeleo kuishia 31, Disemba 2017

| Na | Jina la Mradi                           | Fedha pangwa         | Fedha tolewa            | Fedha tumika            |
|----|---|----------------------|-------------------------|-------------------------|
| 1  | Miradi ya Mapato ya Ndani (60%)         | 1,237,427,000        | 111,898,316             | 111,898,316             |
| 2  | Rural Water Supply and Sanitation       | 3,935,836,000        | 140,621,033.53          | 137,418,823.53          |
| 3  | Health Sector Basket Fund (HSBF)        | 959,931,000          | 239,982,750             | 37,272,900              |
| 4  | Local Govt. Capital Devt. Grant (LGCDG) | 1,776,225,000        | 0                       | 0                       |
| 5  | Mfuko wa Jimbo (CDCF)                   | 67,917,000           | 67,917,000              | 67,917,000              |
| 6  | Capitation Secondary                    | 79,040,000           | 55,774,911              | 55,774,911              |
| 7  | School Meals Secondary                  | 50,537,000           | 30,189,034              | 30,189,034              |
| 8  | Fidia ya Ada Shule za Kutwa Sec         | 180,680,000          | 93,249,755              | 93,249,755              |
| 9  | Head Masters Allowance SEC              | 69,000,000           | 28,750,000              | 28,750,000              |
| 10 | Capitation Prim School                  | 351,225,000          | 248,525,656             | 248,525,656             |
| 11 | Special School Prim School              | 101,314,000          | 60,194,862              | 60,194,862              |
| 12 | Ward Educ. Coordinators Prim School     | 81,000,000           | 20,250,000              | 20,250,000              |
| 13 | Head Teachers Allowance Prim School     | 331,200,000          | 82,800,000              | 82,800,000              |
| 14 | TASAF                                   | 0                    | 1,831,046,882.05        | 1,725,056,491           |
|    | <b>Jumla Kuu</b>                        | <b>9,021,332,000</b> | <b>3,011,200,199.58</b> | <b>2,699,297,748.53</b> |

## **2.6 MAFANIKIO**

### **Sekta ya Elimu Sekondari**

1. Tumefanikiwa kuongeza idadi ya vyumba vya madarasa toka 202 hadi kufikia 206 kati ya vyumba vya madarasa 270 vinavyohitajika
2. Tumekamilisha vyumba 2 vya maabara katika shule ya sekondari ya Misasi na Misungwi na hivyo kufanya vyumba vilivyokamilika kufikia 7. Jumla ya mahitaji yote ni vyumba 69. Vilivyokamilika ni 7 na 62 viko hatua ya ukamilishaji
3. Tumefanikiwa kuanzisha ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya uanzishwaji wa masomo ya kidato cha tano katika shule za Misasi na Paulo Bomani. Katika shule ya sekondari Misasi ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa uko hatua ya boma na katika shule ya sekondari Paul Bomani vyumba viwili vya madarasa vimefanyiwa ukarabati na vimekamilika.
4. Tumefanikiwa kuanzisha ujenzi wa miundombinu ya vyumba vya madarasa na majengo ya utawala katika shule za sekondari tarajiwa za Gulumungu, Nyang'homango na Nkorati
5. Tumefanikiwa kuanzisha masomo ya TEHAMA katika shule za sekondari Sanjo, Idetemya na Mawe Matatu kati ya shule 23 za sekondari zilizopo
6. Tumefanikiwa kuongeza idadi ya walimu wa sayansi toka 110 hadi 145 kati ya walimu 235 wa sayansi wanaohitajika
7. Tumefanikiwa kupandisha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya kitaifa kutoka 71% hadi 75.3% katika matokeo ya mtihani wa kidato cha nne 2016 na kuwa nafasi ya 3 katika wilaya 8 za Mkoa wa Mwanza.

### **Sekta ya Kilimo**

1. Idara imefanikiwa kuandikisha wakulima 24,665 wa pamba kwa msimu wa kilimo 2017/2018, lengo lilikuwa kuandikisha wakulima 54,093.
2. Zimesambazwa mbegu za pamba kiasi cha tani 502 katika vijiji 113. Hii ni sawa na 88% ya lengo ambalo ni tani 570
3. Katika msimu 2017/2018 wilaya iliweka lengo la kulima ekari 57,000 za pamba, mpaka sasa zimepandwa ekari 39,871 sawa na asilimia 70%
4. Elimu imetolewa kwa vikosi kazi 113 na wakulima wawezeshaji 226 juu ya majukumu yao katika kusimamia zao la pamba
5. Zimenunuliwa pikipiki nne (4) kwa ajili ya kusimamia shughuli za kilimo na kutoa huduma za ugani katika tarafa za Misungwi, Mbarika, Inonelwa na Usagara. Pikipiki hizo zitakuwa chini ya Afisa Tarafa.

## **Sekta ya Mifugo**

1. Zoezi la upigaji chapa kwa ng'ombe limetekelezwa kwa 122.7%, ng'ombe 160,996 zimepigwa chapa na kuweka lengo la ng'ombe 131,250
2. Mifugo haramu imedhibitiwa kwa 100% kutoka ng'ombe 22,500 zinazohamia toka wilaya za jirani kufuata malisho maeneo ya kandokando ya ziwa hadi 0%
3. Chanjo za kuku kideri idadi y wafugaji wanaochanja imeongezeka kutoka 25% - 45%
4. Magonjwa ya mifugo yaenezayo na kupe yamedhibitiwa uogeshaji toka 45% ya ng'ombe wote hadi 60% kwa kutumia majosho na pump

## **Sekta ya Maji**

1. Kufanya ukarabati wa miundombinu ya Mradi wa Maji bomba Fella
2. Kufanya ukarabati wa visima vya kina kirefu katika vijiji vya Mitindo (Hospitali ya Mitindo), Mondo 1 (Mwaniko sekondari), Mwambola 1(Kitongoji cha Budutu) Nyamatala 1,Usagala 1(Misungwi), Gambajiga 1, Nange 1, Mitindo A 1, Kanyelele 1, Mbarika (mradi wa Maji bomba), Ngaya Ngaya 1, Ng'ombe 2, Misungwi Mitindo 1,Milembe Sekondari 1, Kasololo 1, Ngudama 1, Gambajiga 2, Mwaniko 1, Lubuga 1, Mbela 1 na Misungwi B 1 na kurejesha huduma ya maji kwa wananchi wa maeneo husika.
3. Kwa kushirikiana na Mashirika ya kidini tumefanikiwa kuchimba visima virefu 2 na vifupi 6 katika vijiji vya Isuka kisima 1, Kifune kisima 1, Lukanga kisima 1, Usagala kisima 1, Ngereka kisima 1, Ibongoya B visima 2 na Songiwe kisima1.
4. Tumefanikiwa kuchimba kisima kirefu na kufunga pampu ya umeme katika shule msingi maalum (Mitindo) kwa fedha za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi na Kisima hicho kimekamilika kuchimbwa na kinatoa huduma ya maji safi na salama kwa watoto wa shule maalum ya Mitindo. Pia tumesimamia ujenzi wa matenki ya kuhifadhi maji na ukarabati wa miundombinu ya kusambaza maji katika shule hiyo.
5. Tumefanikiwa kuunda vyombo/Jumuiya za Watumiaji Maji 10 katika vya vijiji vya Kasololo, Sumbugu, Matale, Ngaya, Igege, Mwawile, Isenengeja, Lubili, Ilalambogo na Nyamatala.
6. Tumefanikiwa kuandaa makisio ya gharama ya mradi wa maji wa Mbarika - Ngaya na kukiwezesha kitengo cha manunuzi kutangaza ili kupata mkandarasi wa kutekeleza mradi huo.
7. Kufanya ukarabati katika mradi wa maji bomba usagara na kurejesha huduma ya maji

## **Sekta ya Afya**

1. Tumefanikiwa kuvuka malengo ya uchanjaji, ambapo tulikuwa na walengwa 8932, tukafanikiwa kuchanja watoto 9321 sawa na asilimia 104%.
2. Huduma za mikoba vituoni zimeongezeka kutoka 95% hadi 100%
3. Kaya zenye vyoo zimeongezeka kutoka 42.2% hadi 72.27%.
4. Wateja 213 waliyoshindwa kuhudhulia kiliniki kwa kipindi cha mwezi 1 mpaka 3 wamerudishwa katika vituo vya huduma

5. Tumefanikiwa kupima vvu kwa watu 10204, wajawazito 3131 na watoto 91 waliyozaliwa na akina mama wenye vvu wamepimwa vvu na kuanzishiwa NVP syrup
6. Vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kutoka vifo 52 hadi vifo 36
7. Tumepunguza vifo vya watoto wachanga kutoka vifo 85 hadi vifo 20
8. Kwa sasa kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa Malaria kimeshuka kutoka 24.6% (Januari – June 2017) hadi 9.5% (Julai – Desemba 2017)
9. Idara ililenga kugawa vyandarua kwa watoto 8,081. Jumla ya watoto 8,822 ambayo ni 109% mpaka desember 2017

## **2.7 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA**

1. Fedha nyingi za Utekelezaji wa Miradi na Shughuli nyingine za Maendeleo kwa Mwaka 2017/2018 kuchelewa kutolewa, hivyo kuathiri shughuli zilizopangwa kwa Mwaka
2. Uhaba wa Ofisi, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ilianzishwa mwaka 1995 tangu Mwaka huo hadi sasa inatumia Jengo la Mkuu wa Wilaya ambapo Ofisi hazijitoshelezi. Hii inasababisha utoaji wa huduma kwa Wananchi kuwa hafifu,
3. Upungufu wa Magari, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ina upungufu mkubwa wa Magari. Magari yaliyopo kipindi chake cha utumiaji kimeshapitwa na wakati, hivyo kutumia gharama kubwa katika matengenezo,
4. Wananchi kuhujumu miradi ya Maji
5. Wananchi bado wanachukulia kuwa huduma ya maji ni bure

## **2.8 MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO**

1. Halmashauri imeomba Maombi Maalum ya kununua Magari ili kupunguza tatizo la Ukosefu wa Magari
2. Halmashauri itaandika barua kwa Katibu Mkuu Hazina kukumbushia fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambayo haijapokea fedha hadi sasa
3. Halmashauri imeomba Maombi Maalum kwa ajili ya Ujenzi wa Jengo la Halmashauri
4. Wanachi tunaendelea kuwa elimisha juu ya utunzaji wa miradi ya maji na kutambua miradi hiyo ni mali yao.
5. Tunaendelea kushauri wizara ili fedha zitolewe kwa wakati na miradi itekelezwe kwa wakati.
6. Serikali iendelee kutenga fedha za uhamasishaji juu gharama za uendeshaji na matengenezo ya miradi.

### 3.0 MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA BAJETI YA MWAKA 2018/2019

Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi inakadiria kutumia jumla ya Tshs. **50,128,248,855** katika kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwemo Miradi ya Maendeleo. Mapato yanayotegemewa Kukusanywa na Kupokelewa ni kama ifuatavyo:-

|                                    |                       |
|------------------------------------|-----------------------|
| i. Mishahara                       | 37,991,598,000        |
| ii. Matumizi ya kawaida (OC)       | 2,836,637,670         |
| iii. Miradi ya Maendeleo           | 6,891,242,185         |
| iv. Mapato ya Ndani ya Halmashauri | 2,408,771,000         |
| • Miradi ya maendeleo (40%) -      | 804,180,400           |
| • Matumizi ya kawaida (60%) -      | 1,604,590,600         |
| <b>Jumla Kuu</b>                   | <b>50,128,248,855</b> |

Mapendekezo ya Bajeti ya Mwaka 2018/2019 yameongezeka kwa kiasi cha Tshs. 8,996,320,855 kutoka 41,131,928,000 Mwaka 2017/2018 hadi Tshs. 50,128,248,855 mwaka 2018/2019. Ongezeko hili limesababishwa na Mambo yafuatayo:-

1. Makadirio ya Makusanyo ya Mapato ya Ndani kwa mwaka 2017/2018 ilikuwa Tshs. 2,062,378,000, Mwaka 2018/2019 imekadiriwa kukusanya Tshs. **2,408,771,000** ambapo kuna ongezeko la Tshs. 346,393,000
2. Mishahara imeongezeka kutoka 29,926,083,000 hadi 37,991,598,000 kuwa na ongezeko la Tshs. 7,780,143,000 hii imetokana na (annual increment, promotion, ajira mpya)

**(i) SURA YA BAJETI :-**

| <b>Chanzo</b>  | <b>Makisio 2018/2019</b> |
|--|--------------------------|
| <b>Mapato ya Ndani ya Halmashauri</b>  |                          |
| a) Mapato ya Ndani   | 2,408,771,000            |
| <b>Jumla mapato ya ndani</b>   | <b>2,408,771,000</b>     |
|  |                          |
| <b>Fedha za Ruzuku</b>   |                          |
| a) Mishahara   | 37,991,598,000           |
| <b>Jumla ndogo</b>   | <b>37,947,618,000</b>    |
|  |                          |
| <b>b)Matumizi ya kawaida (OC)</b>  |                          |
| a. Ruzuku ya Fidia (GPG)   | 136,187,000              |
| b. Utawala   |                          |
| • Mipango  | 10,068,000               |
| • Ukaguzi wa Ndani   | 10,068,000               |
| • Maendeleo ya jamii   | 6,711,000                |
| • Maliasili  | 6,711,000                |
| • Ushirika   | 6,711,000                |
| • Biashara   | 6,711,000                |
| • Ardhi  | 6,711,000                |
| • Mazingira  | 6,711,000                |
| c. Elimu Sekondari   | 654,889,670              |
| d. Elimu msingi  | 1,611,420,000            |
| e. Afya  | 304,968,000              |
| f. Maji  | 14,623,000               |
| g. Ujenzi  | 16,022,000               |
| h. Kilimo & Mifugo   |                          |
| • Kilimo   | 22,875,600               |
| • Mifugo   | 15,250,400               |
| <b>Jumla ndogo- Ruzuku (OC)</b>  | <b>2,836,637,670</b>     |
| Miradi ya Maendeleo  | 6,891,242,185            |
| <b>Jumla ndogo Miradi ya Maendeleo</b>   | <b>6,891,242,185</b>     |
| <b>Jumla Kuu Matumizi ya Kawaida, Mishahara na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2018/2019</b> | <b>50,128,248,855</b>    |

**(ii) MUHTASARI WA MAPENDEKEZO YA MAKISIO YA MISHAHARA 2018/19**

Katika mwaka 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya inakadiria kutumia jumla ya shs **37,991,598,000** kwa ajili ya kugharamia Mishahara ya Idara za Halmashauri ya Wilaya. Mchanganuo wa Makisio hayo Kiidara ni kama ifuatavyo:-

| <b>KASMA</b> | <b>SEKTA</b>                     | <b>KIWANGO</b>        |
|--------------|----------------------------------|-----------------------|
| 5004         | Mishahara ya GS2 na Juu          | 2,495,271,000         |
| 5006         | Elimu - Utawala                  | 286,743,000           |
| 5007         | Elimu - Shule za msingi          | 18,902,232,000        |
| 5008         | Elimu Sekondari                  | 7,330,425,000         |
| 5010         | Afya - Tiba                      | 1,250,715,000         |
| 5011         | Afya - Kinga                     | 431,346,000           |
| 5012         | Vituo vya Afya                   | 2,244,720,000         |
| 5013         | Zahanati                         | 2,053,233,000         |
| 5014         | Miundo Mbinu                     | 285,165,000           |
| 5017         | Maji Vijijini                    | 282,963,000           |
| 5031         | Mishahara ya Watendaji wa Vijiji | 408,906,000           |
| 5033         | Kilimo& Mifugo                   | 2,019,879,000         |
|              | <b>JUMLA KUU MISHAHARA</b>       | <b>37,991,598,000</b> |

**(iii) MUHTASARI WA MGAO WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

Katika mwaka 2018/2019, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tshs. **9,717,786,015** kwa ajili ya Utekelezaji wa Shughuli za Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Tshs. **2,648,322,400** ni Fedha za Ndani na Tshs. **7,069,463,615** ni Fedha za Nje. Fedha hizi zimepangwa kutekeleza Miradi/Program Nane (8) kama ilivyoorodheshwa hapa chini:-

| <b>NA</b> | <b>JINA LA MRADI</b>                           | <b>MAKISIO 2018/2019</b> |                      |                      |
|-----------|--|--------------------------|----------------------|----------------------|
|           |  | <b>Ndani</b>             | <b>Nje</b>           | <b>Jumla</b>         |
| 1.        | Program ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini | 0                        | 4,027,169,185        | 4,027,169,185        |
| 2.        | Mfuko wa Afya wa Pamoja (HSBF)                 | 0                        | 959,931,000          | 959,931,000          |
| 3.        | Ruzuku ya Maendeleo (LGCDG)                    | 1,776,225,000            | 0                    | 1,776,225,000        |
| 4.        | Mfuko wa Jimbo (CDCF)                          | 67,917,000               | 0                    | 67,917,000           |
| 5.        | RBF  | 0                        | 1,809,056,430        | 1,809,056,430        |
| 6.        | Own Source                                     | 804,180,400              | 0                    | 804,180,400          |
| 7.        | AGPAH  | 0                        | 160,105,000          | 160,105,000          |
| 8.        | IMMA   | 0                        | 113,202,000          | 113,202,000          |
|           | <b>Jumla miradi</b>                            | <b>2,648,322,400</b>     | <b>7,069,463,615</b> | <b>9,717,786,015</b> |



**MCHANGANUO WA MAPENDEKEZO YA MIRADI YA MAENDELEO  
ITAKAYOTEKELEZWA KWA MWAKA 2018/2019**

**MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA KWA KUTUMIA MAPATO YA NDANI (40%)**

| S/N | Idara           | Mradi pendekezwa  | Fedha pendekezwa 2018/2019 |
|-----|-----------------|---|----------------------------|
| 1   | Fedha           | Ununuzi wa POS 40   | 38,000,000                 |
|     |                 | Kufanya tafiti na tathimini ya vyanzo vya mapato ya ndani   | 25,000,000                 |
|     | Habari/Tehama   | Kuanzisha kituo cha radio ya Misungwi na Ununuzi wa vyombo vya matangazo                                      | 19,080,400                 |
| 2   | Mipango         | Uchangiaji wa Mradi ya Maendeleo katika ngazi ya Halmashauri na Ngazi za vijiji                               | 30,000,000                 |
| 3   | Utawala         | Ujenzi wa ukumbi na ofisi za Halmashauri  | 100,000,000                |
|     |                 | Ukarabati wa nyumba 8 za watumishi  | 25,000,000                 |
|     |                 | Kuimarisha mfumo wa Takwimu katika ngazi zote.  | 25,000,000                 |
|     |                 | Maandalizi ya Mipango, Bajeti na taarifa za LAAC  | 50,000,000                 |
|     |                 | Ujenzi wa Kibanda cha Walinzi Halmashauri   | 3,500,000                  |
|     |                 | Ukamilishaji wa uzio wa nyumba ya Mkurugenzi  | 15,000,000                 |
| 4   | Kilimo          | Kuwezesha uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula kwa kununua trekta 2@50,000,000 na pikipiki 27@1,800,000 | 148,600,000                |
| 5   | Mifugo na Uvuvi | Kujenga kiwanda cha kuchakata ngozi Misungwi  | 55,000,000                 |
| 6   | Elimu Msingi    | Ukarabati /Ukamilishaji wa vyumba vya Madarasa na Nyumba za Walimu na Vyoo                                    | 40,000,000                 |
| 7   | Elimu Sekondari | Ukarabati wa vyumba 20 vya madarasa katika shule za sekondari za Sanjo na Misasi                              | 40,000,000                 |
| 8   | Ardhi           | Shughuli za mipango miji na upimaji   | 10,000,000                 |
|     |                 | Kulipa Fidia ya ardhi kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na stendi                                    | 90,000,000                 |
|     |                 | Kufanya Uthamini wa Majengo ili kutoza kodi ya Majengo  | 10,000,000                 |
| 9   | Mazingira       | Kuanzisha Bustani ya Miti ya Halmashauri ya Wilaya yenye uwezo wa Kuzalisha miche miti zaidi                  | 5,000,000                  |

|    |       |  |                    |
|----|-------|--|--------------------|
|    |       | ya 60,000 na kutoa elimu ya upandaji miti ifikapo Juni 2019  |                    |
|    |       | Kununua Vifaa vya Kuzolea na Kutunzia Taka Ngumu na Kuvisambaza katika Mji wa Usagara, Misungwi, Misasi na Kigongo Ifikapo Juni 2019   | 5,000,000          |
| 10 | Nyuki | Kununua Mizinga ya Kufugia Nyuki 60 na Kuwezesha 4 Vikundi vya ujasilimali kwaajili ya Ufugaji wa Nyuki katika Misitu ya Hifadhi Kutoka Kijiji cha Mwakitolyo, Mwambola, Mwaniko na Lubuga ifikapo Juni 2019 | 3,600,000          |
|    |       | Kununua Vifaa vya Kujikinga vya Ufugaji wa Nyuki kama mavazi, Bomba la moshi na kofia na Kusambaza kwenye Vikundi 4 vya Mwaniko, Mwakitolyo, Mwambola na Lubuga ifikapo Juni 2019                            | 1,400,000          |
| 11 | Afya  | Kujenga jengo la kuhifadhi Maiti katika hospitali ya Wilaya ya Misungwi  | 40,000,000         |
| 12 | Maji  | Ukarabati wa mradi wa maji wa Matale - Igongwa - Kwimwa  | 25,000,000         |
|    |       | <b>Jumla Kuu Miradi ya Own Source</b>  | <b>804,180,400</b> |

**MIRADI KUPITIA RUZUKU YA MAENDELEO - CDG**

| <b>Na</b> | <b>JINA L MRADI NGAZI YA WILAYA</b>  | <b>GHARAMA ZA MRADI</b> |
|-----------|--|-------------------------|
|           | <b>MIRADI YA NGAZI YA WILAYA (50%)</b>   |                         |
| 1.        | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Maegesho ya magari makubwa Stendi ya mabasi Misungwi | 70,490,000              |
| 2.        | Ujenzi wa vibanda 25 vya biashara katika soko la Misungwi                      | 75,000,000              |
| 3.        | Ujenzi wa vibanda 50 vya biashara katika soko la Mifugo Nyamatala - Ng'ombe    | 150,000,000             |
| 4.        | Ujenzi wa Ukumbi wa mikutano na Ofisi 5 za Halmashauri                         | 200,000,000             |
| 5.        | Ujenzi wa nyumba ya mtumishi daraja la kwanza                                  | 80,000,000              |
| 6.        | Ujenzi wa kituo cha Radio  | 50,000,000              |
| 7.        | Ujenzi wa choo matundu 8 na bafu 4 katika soko la Misungwi                     | 25,000,000              |
| 8.        | Ujenzi wa vibanda 20 vya biashara katika Stendi ya mabasi madogo Nyashishi     | 60,000,000              |
|           | <b>JUMLA NGAZI YA WILAYA</b>   | <b>710,490,000</b>      |
|           | <b>MIRADI NGAZI YA VIJJI NA KATA (50%)</b>                                     |                         |
| 9.        | Miradi ya maji   | 40,000,000              |
| 10.       | Miradi ya Kilimo   | 40,000,000              |
| 11.       | Miradi ya Mifugo na Uvuvi  | 20,490,000              |
| 12.       | Miradi ya Mazingira  | 10,000,000              |
| 13.       | Miradi ya Nyuki  | 10,000,000              |
| 14.       | Ujenzi wa Ofisi 2 za Kata ya Kanyebele na Sumbugu                              | 80,000,000              |
| 15.       | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Ofisi na choo katika Kijiji cha Buhunda              | 10,000,000              |
| 16.       | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Ofisi na choo katika Kijiji cha Ndinga               | 20,000,000              |
| 17.       | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Ofisi na choo katika Kijiji cha Lukanga              | 10,000,000              |
| 18.       | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Ofisi na choo katika Kijiji cha Nange                | 10,000,000              |
| 19.       | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Ofisi na choo katika Kijiji cha Mwasonge             | 10,000,000              |
| 20.       | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Ofisi na choo katika Kijiji cha Lutalutale           | 10,000,000              |
| 21.       | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Ofisi na choo katika Kijiji cha Ngudama              | 10,000,000              |
| 22.       | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Ofisi na choo katika Kijiji cha Nguge                | 10,000,000              |
| 23.       | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Ofisi na choo katika Kijiji cha Isenengeja           | 10,000,000              |
| 24.       | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Ofisi na choo katika Kijiji cha Ilalambogo           | 20,000,000              |
|           | <b>Jumla ndogo</b>   | <b>320,490,000</b>      |
|           | <b>Elimu Sekondari</b>   |                         |
| 1.        | Ukamilishaji wa Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa S/Sekondari Gulumungu          | 40,000,000              |
| 2.        | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Maabara S/Sekondari Mbarika                          | 30,000,000              |
| 3.        | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Maabara S/Sekondari Paul Bomani                      | 60,000,000              |
| 4.        | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Maabara S/Sekondari Kasololo                         | 20,000,000              |
|           | <b>Jumla ndogo</b>   | <b>150,000,000</b>      |
|           | <b>Elimu Msingi</b>  |                         |
| 1.        | Ukamilishaji wa Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa S/Msingi Bunge                 | 20,000,000              |

|    |  |                    |
|----|--|--------------------|
| 2. | Ukamilishaji wa Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa S/Msingi Mwagiligili   | 20,000,000         |
| 3. | Ukamilishaji wa Ujenzi wa nyumba ya Mwalimu S/Msingi Ngw'amazengo  | 20,000,000         |
| 4. | Ukamilishaji wa Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa S/Msingi Mwamhuli  | 20,000,000         |
| 5. | Ukamilishaji wa Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa S/Msingi Mwabuga   | 20,000,000         |
| 6. | Ukamilishaji wa Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa S/Msingi Iteja   | 20,000,000         |
| 7. | Ukamilishaji wa Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa S/Msingi Mwanangwa   | 20,000,000         |
|    | <b>Jumla ndogo</b>   | <b>140,000,000</b> |
|    | <b>Idara ya Afya</b>   |                    |
| 1. | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Zahanati ya Lutalutale   | 10,000,000         |
| 2. | Ukamilishaji wa ujenzi wa Jengo la Zahanati ya Kijiji cha Nyamayinza   | 20,000,000         |
| 3. | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Kwimwa  | 20,000,000         |
| 4. | Upanuzi wa Jengo la Zahanati ya Kijiji cha Mahando   | 20,000,000         |
| 5. | Ukamilishaji wa Ujenzi wa nyumba ya Mganga wa Zahanati ya Ibinza   | 10,000,000         |
| 6. | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Ng'obo  | 20,000,000         |
|    | <b>Jumla ndogo</b>   | <b>100,000,000</b> |
|    | <b>Jumla ya Miradi ngazi ya Vijiji na Kata</b>   | <b>710,490,000</b> |
|    | <b>Ufuatiliaji na Tathimini kwa Ngazi ya Wilaya (10%)</b>  |                    |
| 1. | Kuwezesha uandaaji wa taarifa za utekelezaji za robo 4 za miradi ya Maendeleo ifikapo 30 Juni 2019.  | 25,000,000         |
| 2. | Kuwezesha uandaaji wa taarifa za robo mwaka, nusu mwaka na mwaka za miradi ya Maendeleo na kuziwasilisha ngazi zinazohusika ifikapo 30 Juni 2019.                            | 9,000,000          |
| 3. | Kuwezesha maandalizi ya upimaji wa vigezo kwa Kata 27, Vijiji 113 na ngazi ya Halmashauri kufanyika ifikapo 30 Juni 2019.  | 8,538,050          |
| 4. | Kuwezesha kitengo cha Ukaguzi wa Miradi ya LCDG ya mwaka wa fedha 2018/19 ifikapo 30 Juni 2019.  | 3,088,050          |
| 5. | Kuwezesha maandalizi na uwasilishaji Mipango, Bajeti za jamii na wilaya mwaka wa fedha 2018/2019 na kuwasilisha kwa Katibu Tawala wa Mkoa na Wizara husika ifikapo Juni 2019 | 28,385,150         |
| 6. | Kuwezesha upatikanaji wa Takwimu kupitia uanzishwaji wa Mfumo wa Takwimu wa Wilaya ifikapo Juni 2019.  | 14,800,000         |
|    | <b>Jumla ndogo</b>   | <b>88,811,250</b>  |
|    | <b>Ufuatiliaji na Tathimini kwa Ngazi ya Vijiji (10%)</b>  |                    |
| 1. | Kuwezesha vijiji 113 na Kata 27 katika usimamizi na maandalizi ya Bajeti kwa kutumia mfumo wa fursa na vikwazo (O & OD) ifikapo 30 Juni 2019                                 | 34,745,000         |
| 2. | Kuwezesha vijiji 113 na Kata 27 kutambua na kuchambua Jitihada za Jamii kwa Mwaka wa fedha 2018/19 ifikapo 30 Juni 2019  | 17,800,000         |
| 3. | Kuwezesha wataalamu wa vijiji 113 na Kata 2 kufanya ufuatiliaji wa shughuli za Maendeleo ifikapo 30 Juni 2019  | 15,676,100         |
| 4. | Kuwezesha wataalamu wa Vijiji 113 na Kata 27 kusimamia na kuandaa taarifa za robo na takwimu za Kisekta na kuziwasilisha ngazi ya Wilaya ifikapo 30 Juni 2019                | 20,590,150         |

|     |  |                      |
|-----|--|----------------------|
|     | <b>Jumla ndogo</b>   | <b>88,811,250</b>    |
|     | <b>Kujenga Uwezo (Capacity Building 10%)</b>   |                      |
| 1.  | Kuwajengea uwezo watendaji wa kata 27 na watendaji wa vijiji 113 juu ya uendeshaji vikao vya kamati za maendeleo ya kata (WDC) kwa kuzingatia utawala bora ifikapo Juni 30 2019. | 19,430,000           |
| 2.  | Kuwezesha maafisa utumishi 3 na maafisa TEHAMA 2 kupata mafunzo ya muda mfupi na mrefu yanayolenga uboreshaji wa taaluma zao ifikapo Juni 30 2019.                               | 12,000,000           |
| 3.  | Kuwezesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu yanayolenga uboreshaji wa taaluma za makatibu muhtasi 5 na watunza kumbukumbu 2 ifikapo Juni 30 2019.                                   | 9,000,000            |
| 4.  | Kuwezesha ununuzi wa samani za ofisini katika ofisi 5 za kata na ofisi 15 za vijiji ifikapo 30 Juni 2019   | 18,979,500           |
| 5.  | Kuwezesha mafunzo ya siku 1 ya mabaraza ya Kata 27 na vijiji 113 ifikapo 30 Juni 2019. kwa watendaji   | 17,850,000           |
| 6.  | Kuwezesha mafunzo ya siku 1 kwa wah. Madiwani 36 na Mh. Mbunge 1 katika uongozi na utawala bora ifikapo 30 Juni 2019.  | 14,850,000           |
| 7.  | Kuwezesha utoaji wa maelekezo ya awali (Induction) na maadili ya kiutumishi kwa waajiriwa wapya 100 ifikapo 30 Juni 2019.  | 7,900,000            |
| 8.  | Kuendesha mafunzo kwa watendaji wa kata 27 na watendaji wa vijiji 113 katika sheria na kanuni za utumishi wa umma ifikapo 30 Juni 2019.  | 19,430,000           |
| 9.  | Kuwapatia mafunzo ya uongozi na utawala bora wenyeviti wa vijiji 113 ifikapo 30 Juni 2019.   | 30,063,000           |
| 10. | Kuwawezesha watendaji wa kata 27 kutambua wajibu na majukumu yao ifikapo 30 Juni 2019.   | 11,160,000           |
| 11. | Kuvijengea uwezo vijiji 113 kutambua fursa na vikwazo vya maendeleo ifikapo 30 Juni 2019.  | 16,960,000           |
|     | <b>Jumla Capacity building</b>   | <b>177,622,500</b>   |
|     | <b>Jumla Kuu</b>   | <b>1,776,225,000</b> |

## MIRADI YA MFUKO WA JIMBO

| Na | Jina la mradi  | Lengo la mradi  | Fedha pangwa      |
|----|--|---|-------------------|
| 1  | Ukamilishaji wa Shule za Msingi kupitia Mfuko wa Jimbo         | Kukamilisha Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa katika Shule za Msingi Wilayani | 22,639,000        |
| 2  | Ukamilishaji wa Zahanati kupitia Mfuko wa Jimbo                | Kukamilisha ujenzi wa Miundombinu katika Sekta ya Afya                    | 22,639,000        |
| 3  | Ukamilishaji wa Ofisi za kata na vijiji kupitia Mfuko wa Jimbo | Kukamilisha ujenzi wa ofisi za vijiji na kata wilayani Misungwi           | 22,639,000        |
|    |  | <b>JUMLA KUU</b>  | <b>67,917,000</b> |

**PROGRAMU YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI**

| NA | JINA LA MRADI   | LENGO LA MRADI  | ENEO LA MRADI   | FEDHA PANGWA   |
|----|---|---|---|----------------|
| 1. | Ukamilishaji wa ujenzi wa mradi wa maji bomba Matale - Manawa - Misasi                      | Kukamilisha ujenzi wa mradi wa maji ya bomba Matale - Manawa - Misasi                       | Matale, Manawa & Misasi   | 344,826,185.28 |
| 2. | Ukamilishaji wa ujenzi wa mradi wa maji bomba Mbarika- Ngaya                                | Kukamilisha ujenzi wa mradi wa maji ya bomba Mbarika- Ngaya                                 | Mbarika, Lutatutale, Nyamamba/Bugisha and Ngaya   | 400,000,000    |
| 3. | Ukamilishaji wa ujenzi wa Mradi wa Maji bomba Kijima - Isakamawe                            | Kukamilisha ujenzi wa mradi wa maji ya bomba Kijima - Isakamawe                             | Kijima na Isakamawe   | 1,200,000,000  |
